

Ramadan Message by President George W. Bush (Swahili)

Napeleka salamu kwa Waislamu wote nchini Marekani na duniani kote wakati huu wa mwezi mtukufu wa Ramadan.

Ramadan ni muda mtukufu katika dini ya kiislamu kuadhimisha kutolewa kwa Quran tukufu kwa mtume Mohammed. Mwezi huu wa kutafakari unatowa fursa kwa waislamu kuzingatia imani yao ya dini na kutekeleza amri za Mungu. Kwa njia ya kufunga, kusali, kujiangaza na kutowa zaka, Waislamu duniani kote wanathibitisha tena nia yao ya dhati ya kuendeleza maisha ya uaminifu, heshima na unyenyekevu.

Katika historia yetu, watu wa madhehebu mbali mbali wameendeleza tabia ya taifa letu. Uislamu ni dini ya amani , na watu wanaofuata imani ya kiislamu wametowa mchango mkubwa kwa taifa letu na kwa dunia. Sisi Wamarekani, tunatukuza uhuru wetu wa kuabudu na tunabakia na nia ya dhati ya kukaribisha watu wa dini zote. Kwa kufanya kazi pamoja kuendeleza uhuru na uelewano, tunajenga hali bora ya baadaye ya matumaini na fursa.

**Mke wangu Laura anaungana nami kuwatakia
kila la heri. Ramadan Mubarak.**